## MASPA - Huduma kwa Wateja kwa wahamiaji

## Kuhusu Maspa

Huduma ya Maspa hutoa mwongozo wa uhamiaji, ushauri na huduma za kitaalamu kwa wahamiaji wote katika manispaa ya Hyvinkää, Järvenpää, Nurmijärvi na Tuusula. Huduma yetu ni bure kwa yeyote anayehitaji msaada. Ikiwa ni lazima, tunatumia mkalimani.

Kwenye tovuti hii (www.maspa.fi) utapata viungo muhimu na taarifa kuhusu huduma zifuatazo

- Jinsi ja kuomba kibali cha makazi hapa Ufini
- Ajira au jinsi ya kuomba furza za mafunzo
- Jinsi ja kutafuta shule na malezi ya watoto
- mambo yanayohusiana na makazi
- huduma za kijamii na afya
- huduma za wataalamu wa ofisi za ujumuishaji wa manispaa
- huduma zingine za serikali

Ikiwa unahitaji huduma katika lugha yako ya kimama au hukupata habari kwenye tovuti hii - tafadhali tembelea ofisi ya ujumuishaji iliyo karibu nawe. Chini ya ukurasa huu utapata maeleza na mawasiliano ja manispaa

## Ifuatayo ni mifano ya huduma, miongozo na aina baribari za ushauri unoyoweza kupokea kupitia huduma za Maspa.

## KELA

Kela, Taasisi ya Bima ya Kijamii ya Ufini.

- Tunasaidia wateja kuelewa maamuzi ya KELA

- Tunasaidia unahitaji kuombaa manufaa mtandaoni
- Tunasaidia unapohitaji kuweka miadi kwa KELA
- Tutakuelekeza hadi ofisi ya KELA iliyo karibu nawe

Kwa habari zaidi kuhusu huduma zinazotolewa na Kela
https://www.kela.fi/web/en

## Usajili

Migri - Huduma ya Uhamiaji ya Finland ni shirika la kufanya maamuzi katika masuala yanayohusiana na uhamiaji, hifadhi, hali ya ukimbizi na uraia.

- Tunapeana mwongozo katika masuala yanayohusiana na vibali vya kuishi - Migri
- Tunasaidia wateja kuelewa maamuzi ya kibali cha makazi
- Tunasaidia unapohitaji usaidizi wakati wa mchakato wa kuomba kibali cha ukaaji
- Tunapeana ushauri kuhusiana na masuala ya kuunganisha familia
- Tunasaidia kama unahitaji usuadizi kuweka miadi kwa Migri
- Tunapeana ushauri jinsi ja kuomba kitambulisho kutoka kwa kituo cha Polisi

Huduma ya uhamiaji ya Kifini - Migri mtandaoni

www.migri.fi
www.poliisi.fi

## Kutafuta kazi

TE-palvelut - Ajira ya umma na huduma za biashara. https://tyomarkkinatori.fi/

- Tunapeana ushauri jinsi ya kujiandikisha kama mtafutaji kazi kwa TE-palvelut

## Masuala yanayohusiana na mafunzo na elimu

- Tunatoa taarifa na ushauri kuhusu taasisi za elimu na njia za elimu
- Tunasaidia katika kufanya maombi unapotaka kujiunga na kituo cha shule

- Tunakuelekeza kwenye kozi za lugha ya Kifini

## Masuala ya makazi

- Tunatoa ushauri juu ya makazi
- Tunasaidia katika kujaza maombi ya makazi ya kukodisha
- Tunasaidia unapotaka kubadilisha anwani
- Tunapeana habari kuhusu makabidhiano ya funguo
- Tunakusaidia katika kukamilisha ombi lako la faida ya makazi kwa KELA

## Watoto wa shule

- Tunasaidia wazazi kuandikisha watoto wao shuleni
- Tunatoa taarifa kuhusu mfumo wa shule na elimu ya awali na shughuli za klabu za mchana
- Tunasaidia katika kujaza fomu mtandaoni

## Elimu ya utotoni / malezi ya siku

- Tunasaidia katika usajili
- Tunatoa habari juu ya elimu ya shule ya mapema
- Tunasaidia katika kujaza fomu za mtandaoni

## Huduma za kijamii

- Tunasaidia unapohitaji kutambua huduma mbalimbali za kijamii
- Tunakusaidia kutuma maombi ya usaidizi wa kijamii na manufaa

## Huduma ya afya

Katika eneo la Keski-Uusimaa (Hyvinkää, Järvenpää, Nurmijärvi na Tuusula) utapata huduma za afya kutoka Keusote (www.keusote.fi)

- Tunasaidia wateja kuelewa hati kutoka kwa huduma ya afya
- Tunasaidia katika kuweka miadi kwa ajili ya huduma za afya

Weka muda wa huduma ya afya mtandaoni – Keusote

https://pro.klinik.fi//contact/keusote

## Masuala ya Haki, Forodha na Polisi

Tunapeana ushauri kuhusu masuala yanayohusiana na kupata huduma za haki, desturi na polisi

Keski-Uusimaa Ofisi ya Msaada wa Kisheria

https://oikeus.fi/oikeusapu/keski-uudenmaanoikeusaputoimisto/en/index.html

## Hobbies na wakati wa bure

- Tunakupa habari kuhusu fursa tofauti za shughuli ya burudani
- Tunakusaidia kuweka usajili mtandaoni.

## Kadi ya ushuru

- Tunakushauri jinsi ya kupata kadi ya ushuru

Pata kadi ya ushuru mtandaoni kutoka kwa huduma ya vero.fi

https://www.vero.fi/en/individuals/tax-cards-and-tax-returns/tax_card/

- Ukiwa na haja tutakuelekeza katika ofisi ja Vero

## Huduma za benki

- Tunakushauri jinsi ya kufungua akaunti ya benki ya Kifini.
- Tunakusaidia kutambua huduma mbalimbali zinazotolewa na benki

## Huduma za bima

Tunatoa ushauri ni wapi unawezapata bima. Kwa mfano  bima ya nyumba au magari

Maelezo zaidi kuhusu bima nchini Ufini kutoka tovuti ya Nordic Co-operation

https://www.norden.org/en/info-norden/insurance-finland

Ikiwa hutapata maelezo uliyohitaji kutoka kwa tovuti hii, tafadhali tembelea ofisi ya Wahamiaji iliyo karibu nawe iliyoorodheshwa hapa chini.

**Ofisi za Wahamiaji za Manispaa**

**Hyvinkää, Mosaiikki-talo**
Martinkatu 9, 05800 Hyvinkää
Phone 040 3152063

**Järvenpää, Verso**
Mannilantie 43, 04400 Järvenpää
Phone 040 315 3423

**Nurmijärvi, Koto-info**
Kuonomäentie 2 (3. kerros), 01800 Klaukkala
Phone 040 317 4106

**Tuusula, Maahanmuuttajat**
Koskenmäenpolku 4 D, 04301 Tuusula
Phone 040 315 2063

Jokela kirjasto
Keskustie 20, 05400 Jokela